

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA NANE**

**19 APRILI, 2022**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA NANE – TAREHE 19 APRILI, 2022

#### I. DUA

#### II. MASWALI:

##### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

##### 63. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara inayoanzia Mji wa Kakonko hadi Muhange.

##### WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

##### 64. MHESHIMIWA RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN (CHAKECHAKE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, mgawanyo wa mapato ya Tozo za Miamala upoje kwa pande za Muungano na vipi yataboresha huduma kwa upande wa Zanzibar.

**WIZARA YA AFYA:**

**65. MHESHIMIWA NORA WAZIRI MZERU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea Wahudumu wa kada mbalimbali za Afya nyumba bora ili kuboresha makazi yao.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**66. MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya mzunguko katika makutano ya barabara ya Dar es Salaam, Morogoro na Bagamoyo kuelekea Mlandizi.

**67. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya kutoka Buza – Kilungule hadi Nzasa.

**68. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, upi mkakati wa Serikali wa kuunganisha barabara za Mkoa wa Tanga na Mikoa jirani.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**69. MHESHIMIWA SIMAI HASSAN SADIKI (NUNGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya ukosefu wa magari na nyumba za Askari Polisi Kituo cha Polisi Nungwi.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**70. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE (TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, Serikali haioni haja ya kurejesha Kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Tunduru ili kuimarisha ulinzi.

**WIZARA YA KILIMO:**

**71. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufufua kilimo cha zao la Muhogo katika Mkoa wa Mtwara.

**WIZARA YA MAJI:**

**72. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji katika Kata za Namajani, Mpanyani, Mlingura, Msikisi na Chigululu zilizopo katika Jimbo la Ndanda.

### III. HOJA ZA SERIKALI:

#### WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

*(Majadiliano yanaendelea)*

DODOMA  
19 APRILI, 2022

N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE